THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

LAND TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY (LATRA)

ROAD AND RAILWAY INFORMATION MANAGEMENT SYSTEM [RRIMS]

MUONGOZO WA MTUMIAJI

December, 2020

Yaliyomo

Yaliyomo.....i
Utangulizi.....1
1.1 Kuhusu mfumo wa RRIMS.....1
1.2 Mahitaji ya jumla kwa mtumiaji wa mfumo.....1
1.3 Kufungua akaunti kwenye mfumo.....2
Usajili wa msafirishaji.....5
2.1 Kufanya maombi ya usajili wa msafirishaji.....5
Maombi ya Leseni.....6
3.1 Maombi ya leseni.....6

Utangulizi

1.1 Kuhusu mfumo wa RRIMS

RRIMS ni mfumo wa Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) unaosimamia usajili wa wadau wa usafirishaji pamoja na ukataji leseni wa vyombo ya usafiri vya biashara.

Aina za usajili zinazofanyika katika mfumo huu ni:

a. Usajili wa wasafirishaji
b. Usajili wa madereva
c. usajili wa makondakta na wasaidizi wa gari
d. Usajili wa wamiliki wa mitandao ya usafirishaji

Maombi ya leseni yanayofanyika kwenye mfumo huu ni:

a. Leseni za magari ya mizigo
b. Leseni za magari ya abiria
c. Leseni za usafiri wa kukodi (Tax, Taxi mtandao)
d. Leseni za bodaboda na bajaji

1.2 Mahitaji ya jumla kwa mtumiaji wa mfumo

Ili kuweza kutumia mfumo mtumiaji atatakiwa kuwa na akaunti kwenye mfumo, ambapo mtumiaji anaweza kujifungulia akaunti kwenye mfumo.

Mahitaji ili kufungua akaunti:

1. Kuwa na kompyuta, simu au kifaa chochote chenye uwezo wa intaneti ili kuwweza kuufikia mfumo

2. Kuwa na barua pepe “email”

3. Kwa mtu binafsi kuwa na namba ya kitambulisho chako cha NIDA

4. Kwa kampuni kuwa na namba ya usajili wa kampuni kutoka BRELA

1.3 Kufungua akaunti kwenye mfumo

Ili kufungua akaunti kwenye mfumo fuata hatua hizi nyepesi.

Zingatia: Zoezi hili la kufungua akauti litafanyika mara moja tu baada ya kusajili akaunti utaweza kutumia akauti yako kufanya maoombi ya huduma mbalimbali kutoka LATRA.

Kwa watumiaji binafsi:

i) Nenda kwenye “browser” ya kompyuta au simu yako.

ii) Ingiza linki: **rrims.latra.go.tz** kisha bonyeza “enter”

iii) Mfumo utafunguka na kama bado haujajisajili utaweza kujisajili kwa kubonyeza kitufe cha **jisajili hapa**;



iv) Chagua jisajili kama mtu binafsi

v) Ingiza namba yako ya NIDA: Andika namba yote bila kuacha nafasi au kuweka alama za deshi (-). mfano 1977888999220000 halafu bonyeza “endelea”.

vi) Jibu kwa usahihi maswali kutoka NIDA ili kuthibitisha kitambulisho chako.

vii) Baada ya kuthibitisha taarifa zako itafunguka fomu ya kujisajili, jaza barua pepe “email”, anuani na taarifa nyingine.

Zingatia:

- Jaza “email” iliyo sahihi na unayoweza kuifikia kwani utatumiwa linki ya ku-activate akaunti yako kwenye email utakayoweka.
- Email moja haiwezi kutumika kwenye akaunti Zaidi ya moja.

viii) Email yenye linki ya kuhuisha akauti yako itatumwa kwenye email yako, tafadhali ingia kwenye email yako na kubonyeza linki hiyo..

ix) Baada ya kubonyeza linki ilitotumwa kwenye email yako, mfumo utakuwezesha kuweka nenosiri/nywila “password” unayoitaka.

x) Hapo utakua umekamilisha kujisajili.

xi) Ingia kwenye mfumo kwa kutumia email na nyila yako.

Kwa makampuni:

i) Nenda kwenye “browser” ya kompyuta au simu yako.

ii) Ingiza linki: **rrims.latra.go.tz** kisha bonyeza “enter”

iii) Mfumo utafunguka na kama bado haujajisajili utaweza kujisajili kwa kubonyeza kitufe cha **jisajili hapa**;

iv) Chagua jisajili kama “kampuni”

v) Jaza taarifa za kampuni kwa usahihi, kwenye namba ya cheti weka namba ya usajili wa kampuni kutoka BRELA.

Zingatia:

- Jaza “email” iliyo sahihi na unayoweza kuifikia kwani utatumiwa linki ya ku-activate akaunti yako kwenye email utakayoweka.
- Email moja haiwezi kutumika kwenye akaunti Zaidi ya moja.

vi) Email yenye linki ya kuhuisha akauti yako itatumwa kwenye email yako, tafadhali ingia kwenye email yako na kubonyeza linki hiyo..

vii) Baada ya kubonyeza linki ilitotumwa kwenye email yako, mfumo utakuwezesha kuweka nenosiri/nywila “password” unayoitaka.

viii) Hapo utakua umekamilisha kujisajili.

ix) Ingia kwenye mfumo kwa kutumia email na nyila yako.

Usajili wa msafirishaji

Mdau yoyote (binafsi au kampuni) anayemiliki chombo cha usafirishaji wa abiria au mizigo anatakiwa kujisajili kama msafirishaji kabla ya kufanya maombi ya leseni kwa chombo cha usafiri kwenye mfumo. Usajili huu unafanyika mara moja tu.

Ada za usajili:

- Kwa mtu binafsi usajili huu ni bure (hauna malipo)
- Kwa makampuni, ada ya usajili ni laki moja (100,000/=) na watapatiwa cheti cha usajili wa msafirishaji

2.1 Kufanya maombi ya usajili wa msafirishaji

Hatua:

1. Ingia kwenye akaunti yako kwa “email” na “password” uliyotumia kujisajili
2. Kwenye menyu ya kushoto bonyeza sehemu ya msafirishaji
3. Bonyeza kitufe cha ongeza maombi
4. Jaza taarifa zinazohitajika kwa usahihi kisha bonyeza hifadhi.
5. Weka viambatanisho vinavyohitajika
6. Baada ya kuhakikisha taarifa zako zipo sahihi, bonyeza “wasilisha” ili kutuma maombi yako LATRA.
7. Baada ya kutuma maombi yatapitiwa na maafisa wa LATRA.
8. Kwa kampuni “bill” itatolewa ili kufanya malipo, baada ya kufanya malipo namba ya msafirishaji itatolewa kwa kampuni.
9. Kwa mtumiaji binafsi, usajili ukikamilika utapatiwa namba ya msafirishaji na utaweza kuendelea na maombi ya huduma nyingine za leseni.

Maombi ya Leseni

Maombi ya leseni yanayofanyika kwenye mfumo huu ni:

1. Magari ya mizigo : Leseni hii inahusisha
    - Magari ya mizigo
    - Maguta ya kubebea mizigo e.t.c
2. Magari ya abiria : Leseni hii inahusisha
    - Daladala
    - Mabasi ya ruti za mkoa hadi mkoa
    - Magari ya shule
    - Magari ya kusafirisha watalii (tours) etc
3. Usafiri wa kukodi : Leseni hii inahusisha
    - Ride hailing (Taxi mtandao mfano mfano uber, taxify, little-ride etc),
    - Tax cab (Taxi zinazopaki vituo maalumu) e.t.c
4. Bodaboda na bajaji :
    - Motorcycle (bodaboda)
    - Tricycle (bajaji)
    - Ride hailing (pikipiki mtandao mfano uber, taxify, little-ride etc)

3.1 Maombi ya leseni

Kabla ya kufanya maombi ya leseni hakikisha umejisajili kama msafirishaji.



Hatua za kufuata:

1. Ingia kwenye akaunti yako kwa “email” na “password” uliyotumia kujisajili
2. Kwenye menyu ya kushoto bonyeza sehemu ya maombi ya leseni
3. Chagua aina ya maombi.
4. Bonyeza kitufe cha “ongeza gari”



5. Jaza taarifa zinazohitajika kwa usahihi kisha bonyeza hifadhi.
6. Weka viambatanisho vinavyohitajika, viambatanisho hivyo ni pamoja na:
    - Kadi ya gari
    - Cheti cha ukaguzi wa gari
    - Kava noti ya bima
    - Cheti cha TALA (Kwa magari ya watalii)
7. Baada ya kuhakikisha taarifa na viambatanisho vipo sahihi, bonyeza “wasilisha” ili kutuma maombi yako LATRA.
8. Baada ya kutuma maombi yatapitiwa na maafisa wa LATRA.
9. Baada ya maombi kupitishwa utapokea bili yenye “control number” kwenye mfumo pamoja na ujumbe mfupi “SMS”.
10. Fanya malipo kupitia control number uliyopewa.
11. Ukishafanya malipo leseni yako itakua tayari, tembelea ofisi za LATRA kupata leseni yako.